BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA NNE

Kikao cha Nane – Tarehe 23 Februari, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

20. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Je, ni utaratibu gani ambao unatumika katika kutoa motisha kwa watumishi wa umma wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

81. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara ya Maalum za SMZ:

    Kumekuwa na maombi ya muda mrefu ya kupatiwa Sheha katika

kijiji cha Jozani, shehia ya Kitogani.

(a) Je, unawaeleza nini wananchi wa kijiji cha Jozani.

(b) Je, ni lini utakutana na wananchi hao, ili kuzungumza nao juu ya suala hili.

(c) Je, ni sababu zipi zinazopelekea hadi hii leo kijiji hicho kukosa Sheha.

182. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika eneo la Kianga Meli Saba, daraja la kwanza kutokea meli sita, upande wa kushoto kwenye msikiti wa Ijumaa pembeni ya daraja hilo, mtaa wa Mchanga Mwingi kuingia ndani, kama laini ya saba kutoka barabarani, kuna Baa iliyojengwa katika makaazi ya wananchi na inapiga mziki kwa sauti na pia mziki huo unazidi saa sita za usiku.

(a) Je, kwa kiasi gani uwepo wa Baa hiyo na shughuli zake katika eneo hilo, unakubalika kisheria.

(b) Je, kuna ugumu gani unaoifanya Serikali ishindwe kuifungia Baa hiyo.

(c) Je, Wizara yako imechukua hatua gani ya kukaa na wananchi wa eneo hilo na kuzungumza nao, ili kutoa kero zao dhidi ya uwepo wa Baa hiyo katika makaazi yao.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

122. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Je, tathmini iko vipi juu ya uwekezaji wa soko la utalii kupitia visiwa vidogo vidogo vilivyopo Zanzibar.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

17. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, kuna utaratibu gani wa ufungaji wa hesabu za sekta na taasisi zote za Serikali kwa pamoja (Consolidated Account) ili

kupata hesabu ya jumla kwa Serikali nzima.

143. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Pamoja na juhudi za Serikali za kuanzisha Mfumo Mtandao wa Manunuzi ya Umma (eProZ), bado mfumo huo una changamoto nyingi ambazo taasisi za umma, wakandarasi na wasambazaji wa bidhaa (suppliers) wamekuwa wakizilalamikia.

(a) Je, ni hatua gani ambazo Serikali inazichukua ili kuhakikisha mchakato mzima wa manunuzi unafanyika kikamilifu kwa njia ya kielektroniki.

(b) Je, mfumo wa eProZ unaendana kwa kiasi gani na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2016 na Serikali ina mpango gani wa kuziboresha sheria na kanuni zetu ili kuhakikisha kuwa mfumo huo unakidhi mahitaji na miongozo ya sheria.

(c) Katika kuwezesha matumizi mazuri ya mfumo wa (eProZ), ni namna gani mfumo huo unawawezesha watumiaji kutumia mifumo mingine ya Serikali kama vile ZAN MALIPO na je, kuna jitihada za kuboresha ushirikiano (integration) wa mifumo hii ili kutoa suluhisho bora zaidi kwa watumiaji na taasisi za umma.

## Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

156. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020/2025 iligusia azma ya kujenga vituo vya utamaduni hapa nchini ikiwa ni sehemu ya kuukuza utalii wetu na kuuinua zaidi uchumi wetu.

Je, tathmini iko vipi juu ya azma hii njema kwa taifa letu.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

59. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na jitihada za Serikali za kujenga madarasa katika skuli za jimbo la Pandani, bado mazingira ya kufundishia na kujifunzia hayajaimarika tofauti na majimbo mengine nchini.

(a) Je, ni skuli ngapi za jimbo la Pandani zina vyumba vya

walimu na wafanyakazi.

(b) Je, ni upi mpango wa haraka wa Serikali wa kuzipatia skuli za jimbo la Pandani mazingira bora ya elimu ikiwemo vyumba vya walimu na wafanyakazi hasa katika skuli za msingi za Mjananza, Kiungoni, Maziwani, Shengejuu na Mzambarauni.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuzipatia skuli za jimbo la Pandani vyumba vya ushauri nasaha vyenye faragha na wasaa kwa matumizi ya wanafunzi na walimu.

139. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na jitihada za Serikali katika kutengeneza Muundo wa Utumishi (Scheme of Service) kwa watumishi wa umma, bado kuna changamoto kubwa ya upandishaji wa madaraja kwa wahadhiri katika vyuo vikuu vya Zanzibar.

(a) Je, takwimu inaonyesha ni idadi ya wahadhiri wangapi waliopandishwa madaraja kutoka wahadhiri mpaka kufikia nafasi ya 'Professor' katika vyuo vikuu vya Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

(b) Ni sababu zipi zinazochangia upungufu wa idadi ya Ma 'Professors' katika vyuo vikuu vya Zanzibar.

(c) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuhakikisha kuwa vyuo vikuu vya Zanzibar vinaweza kupandisha madaraja kwa wahadhiri wake na kuhakikisha kuwa kuna idadi ya kutosha ya Ma 'Professors' kwa ufanisi wa taasisi hizi za elimu ya juu.

<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:</u>

31. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Serikali ya Awamu ya Nane kwa nia safi kabisa imeamua kuwasaidia wazee wenye umri wa miaka 70 kwa kuwaongezea pencheni jamii kutoka Tsh. 20,000 hadi 50,000, kwa lengo la kuwapunguzia ukali wa maisha.

(a) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuwapatia wazee hawa stahiki zao hizo.

(b) Kulingana na umri walionao wazee wetu hawa. Je, huo utaratibu unaotumika ni rafiki kwao.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

110. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kombe la Mapinduzi ni kielelezo halisi cha uhuru wa Mzanzibari katika kukuza tasnia ya michezo nchini.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea wananchi kukosa kuangalia fainali za miaka 60 ya mpira wa miguu kupitia televisheni yao pendwa ya ZBC.

(b) Ni yepi matarajio ya fainali zinazofuata kuhusiana na kuoneshwa mubashara katika televisheni ya ZBC.

132. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Je, Sera ya lugha adhimu ya Kiswahili imekwama wapi.

<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

86. MHESHIMIWA MOH’D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa juhudi zake za kuimarisha kilimo katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, lakini pamoja na juhudi zinazoendelea kutekelezwa kwenye bonde la Machigini lililopo katika jimbo la Mtambile, wananchi wanaotegemea shughuli za kilimo katika bonde hilo wanakabiliwa na changamoto ya kutoendelea na shughuli zao za kilimo kupisha uendelezwaji wake.

(a) Je, ni lini wakulima wa bonde la Machigini wataruhusiwa kuendelea na harakati zao za kilimo kama ilivyokuwa awali.

(b) Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kukamilisha hatua zilizofanyika za uimarishaji wa bonde hilo.

(c) Je, sababu gani zilizosababisha kukwama kwa ujenzi wa miundombinu yake.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

16. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa kuwa Kiwanda cha Makonyo cha Wawi Pemba ni cha siku nyingi. Na kwa kuwa Kiwanda hicho kinaendelea kutumika ingawa vifaa vyake vingi vinaonekana kuchakaa, na kwa kuwa Kiwanda hicho ndio tegemeo kubwa la Serikali katika kuchakata baadhi ya bidhaa zinazotokana na karafuu.

Je, ni upi mpango wa sasa wa Serikali katika kukinusuru Kiwanda hicho.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

84. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ujenzi wa barabara ya Mtambile hadi Kangani unaendelea katika hali ya kusuasua licha ya juhudi za mfano zinazochukuliwa na Serikali yetu za kuuingiza ujenzi wa barabara kwenye mpango wa bajeti ya Serikali. Barabara hiyo ipo katika hali ngumu kimatumizi inayowafanya wananchi wa Mtambile kushindwa kuitumia ipasavyo barabara hiyo kwa kuhofia kuharibu vyombo na mali zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka utakaohakikisha ujenzi huo unakamilika.

108. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Bado suala la changamoto ya barabara ya Melinne Makaburini halijapatiwa ufumbuzi.

(a) Je, ni lini hasa Wizara itaifanyia maboresho barabara hiyo kwa muktadha wa ahadi za viongozi wake.

(b) Ni lini barabara ya Taveta Magirisi itafanyiwa ukarabati ili kuwaondolea wananchi usumbufu mkubwa wanaoendelea kuupata.

## III. <u>HOJA ZA KAMATI:</u>

### <u>Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:</u>

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
23 Februari, 2024.

(Raya Issa Msellem)
<u>KATIBU WA BARAZA</u>.